JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI NJOMBE

SHULE YA SEKONDARI YAKOBI,
S.L.P 708,
NJOMBE
Tarehe: 06/11/2020

Jina la Mwanafunzi ……
C/O Mwalimu Mkuu
Shule ya Msingi ……..
Njombe

YAH: **MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YAKOBI HALMASHAURI YA MJI NJOMBE MKOA WA NJOMBE MWAKA 2020.**

1.0 **UTANGULIZI**

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Shule ya sekondari Yakobi (Limage) ipo umbali wa km 23 kusini mwa mji mkuu wa Mkoa/ Halmashauri ya Mji Njombe.

Usafiri wa basi kutoka mjini hadi shuleni unapatikana katika kituo cha mabasi cha Njombe mjini nauli ni kiasi cha shilingi elfu nne (**Tshs 4,000/=).**

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe **06/01/2021** unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **11/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **18/01/2021**.

2.0 **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

2.1 **SARE ZA SHULE**

WASICHANA

a) NGUO ZA DARASANI

- Suruali mbili (02) za rangi ya damu ya mzee namba moja (kitambaa kimeambatanishwa) isiwe ya kubana.
- Vigauni viwili rangi ya damu ya mzee namba moja, mshono umembatanishwa.

- Shati mbili nyeupe zenye kola na mikono mirefu.
- Pluneki nyeupe au rangi ya maziwa.
- Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili (02) vyenye gidamu vya kufunika na vyenye kisigino kifupi na siyo raba, simple, au yebo.
- Hijabu kwa wanafunzi wa kiislamu rangi nyeupe lakini asifuge nywele awe na nywele fupi.
- Soksi nyeupe zisizo na maandishi pea tatu (03).
- Sweta pea mbili (02) rangi ya kijani kibichi angalia rangi ya uzi ulio ambatanishwa (mshono –V- shingo).
- Pedi bunda tano (05)

b) NGUO ZA MICHEZO :

- Raba nyeupe za michezo pea moja (01).
- Traki suti ya bluu yenye ufito mweupe pea moja (01)
- Soksi ndefu rangi yeyote pea mbili (02).
- T-sheti rangi ya bluu nzito isiyo na maandishi (shingo ya duara) pea mbili (02)

c) NGUO ZA KAZI:

- Nguo za ndani za kutosha kuanzia pea tano (05).
- Sketi rangi ya kijani jeshi urefu wa 30cm chini ya goti pea mbili (02) kitambaa na mshono vimeambatanishwa
- Sweta rangi kijani jeshi pea mbili (02).
- Raba rangi yeyote pea moja (01)
- Ndala kwa ajili ya kuogea pea moja (01)

NB; Nguo aina nyingine yeyote hazita ruhusiwa kuvaliwa shuleni, ni marufuku kuja nazo!

<u>WAVULANA</u>

a) NGUO ZA DARASANI

- Suruali pea mbili (02) rangi damu ya mzee namba moja (angalia rangi ya kitambaa kilicho ambatanishwa) isiyobana na ndefu ya kutosha na yenye (turn up) chini.
- Shati mbili nyeupe zenye kola na mikono mifupi.
- Pluneki nyeupe au rangi ya maziwa.

- Viatu nyeusi jozi mbili (02) vyenye gidamu na kisigino kifupi visiwe vya kuchongoka mbele (choma) na isiwe raba.
- Soksi nyeusi pea tatu (03).
- Sweta pea mbili (02) rangi ya kijani kibichi angalia rangi ya uzi ulioambatanishwa

b) NGUO ZA MICHEZO;

- Raba nyeupe pea moja (01).
- T-sheti rangi ya bluu nzito (KOLA ROUND) isiyo na maandishi pea mbili (02)
- Traki suti ya bluu yenye ufito mweupe pea moja (01)
- Bukta ya bluu yenye ufito mweupe pea moja (01)
- Soksi ndefu rangi yeyote pea mbili (02)

c) NGUO ZA KAZI;

- Nguo za ndani za kutosha kuanzia pea tano (05).
- Suruali rangi ya kijani kibichi pea mbili (02) (angalia rangi ya kitambaa kilicho ambatanishwa) isiyobana na ndefu ya kutosha na yenye (turn up) chini.
- Sweta rangi kijani jeshi pea mbili (02).
- Raba rangi yeyote pea moja (01)
- Ndala za kuogea pea moja (01)

Nb; Nguo aina nyingine yeyote hazita ruhusiwa kuvaliwa shuleni, ni marufuku kuja nazo!

2.2 MAHITAJI BINAFSI KWA WAVULANA NA WASICHANA

- Blanketi zito moja (01)
- Mashuka mawili (02) rangi ya pinki
- Godoro la dodoma moja (2.5ft × 6) na mto mmoja (01)
- Ndoo moja (01) amboni au ya mafuta lita ishirini kwa ajili ya matumizi ya jikoni na ndoo moja lita kumi (10) amboni au ya mafuta kwa ajili ya kuogea na kufulia
- Fagio ngumu au laini kwa ajili ya kufagilia (01)
- Kontena lenye patisheni, kikombe, na kijiko kwa ajili ya kulia chakula.
- Gudulia la kuhifazia maji ya kunywa lita tatu au tano (03 au 05)
- Sabuni ya kufulia miche mitano (05) na kuogea medicated (mfano detol, protex, rungu, family, n.k) vipande vitano.

- Mafuta ya kupaka ya mgando ujazo (500g) na sio losheni au mafuta yanayoharibu ngozi (mfano, caroton, maxlight, pure skin, carolight, nk)
- Picha passport size mbili zilizo pigwa hivi karibuni akiwa amevaa sare ya shule.
- Taulo moja (01) wavulana pia wasichana taulo moja (01) na pea moja ya khanga au kitenge
- Kiwi, brashi, dawa ya meno kubwa moja (01), mishwaki miwili (02), leso moja.
- Mvulana aje na **panga** lililonolewa, Msichana aje na **jembe** jipya lenye mpini.

2.3 VIFAA VYA DARASANI

- Madaftari makubwa ya kutosha yasipungue 12 (counter books 3Q).
- Mathematical set (mkebe wa hesabu wenye vifaa vyote), peni ishirini (20pc), penseli tano (05) na awe na begi moja imara la madaftari.
- Aje na "**Spring file"** na **sio "Box file"** moja kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu zake likiwa na (Copy) nakala ya cheti cha kuzaliwa.

2.4 MWANAO ANAPOKUJA SHULENI AJE NA MICHANGO IFUATAYO,

Aina ya mchango	**Mhula wa I**	**Mhula wa II**	**Jumla**
Fedha	**83,000/**	**68,000/**	**151,000/**
Mahindi	**Debe 06**	**Debe 06**	**Debe 12**
Maharage	**Debe 01 na lita 10**	**Debe 01 na lita 10**	**Debe 03**
Mchele	**Lita 10**	**Lita 10**	**Debe 01**
Bunda la karatasi A4	**01**	**---**	**01 kwa mwaka**

Mchango wa fedha tasilimu ulipwe Benki ya **NMB** namba ya akaunti **60602300566** jina la akaunti YAKOBI **SEKONDARI**

NB:

- ***TUNAOMBA MZAZI AU MLEZI KWENYE MCHANGO WA NAFAKA UTULETEE NAFAKA SIO FEDHA.***

3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu na mafunzo ya ufundi, yenye dhamana na elimu nchini na Ofisi ya Rais - TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa;
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote; na
i) Kutunza mali za umma.

3.1 MAKOSA YAFUATAYO YANASABABISHA KUFUKUZWA SHULE.

a) Wizi
b) Uasherati na ushoga.
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
e) Kupigana au kupiga
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
g) Kudharau Bendera ya Taifa
h) Kuwa mjamzito/kupata mimba/kusababisha mimba ndani au nje ya shule.
i) Kuoa au kuolewa

j) Kutoa mimba

k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.

l) Kukataa adhabu kwa makusudi.

m) Utoro

n) Kuwa na simu ya mkononi, laini ya simu, camera,redio, CD na siraha ya aina yoyote.

Nb: Mwanafunzi atakayekamatwa na kosa namba 3.1 (m) licha ya adhabu ya kufukuzwa shule atatakiwa kulipa waya wa umeme roll moja ya 1.5mm na roll moja ya 2.5mm kwa ajili ya kufidia miundo mbinu ya umeme wanayoiharibu kila siku. Mzazi/Mlezi uongozi wa shule unakuomba ukae na mwanao na umshauri juu ya taratibu za shule.

3.2 SHERIA ZA DAHARIA/HOSTEL

Mwanafunzi wa hostel licha ya kufuata sheria zote mhimu za shule na miiko yake hapaswi kufanya yafuatayo:

1. Huruhusiwi kulala nje ya daharia/hostel
2. Huruhusiwi kuja na chakula kilichopikwa nje ya shule
3. Huruhusiwi kulala kwenye bweni/chumba/kitanda ambalo hujapangiwa na mwalimu
4. Huruhusiwi kuja na nguo ambazo hazipo kisheria
5. Huruhusiwi kupiga au kupigana au kutoa vitisho vya aina yoyote kwa mwanafunzi mwenzio
6. Huruhusiwi kulala bwenini muda wa darasani
7. Huruhusiwi kumuibia mwenzio wala kularua tranka lake.

NB: ***Iwapo Mwanafunzi atakutwa na utovu wa nidhamu aina yoyote atatakiwa kulipa trip mbili(02) za mawe/nyaya za umeme roll moja (01) (2.5mm na 1.5mm).***

4.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI

a) Medical examination form' ambayo itajazwa na Mganga mkuu wa hospitali ya serikali tu Hospitali binafsi haitakubaliwa. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
d) Fomu ya kukubali masharti ya hostel

NB: Mwanafunzi anaporipoti shuleni awe na vifaa vyote alivyoagizwa hapa shuleni ikiwemo sare za shule alizoagizwa.

- **Fomu hii ni mali ya shule hivyo basi unaombwa kurudisha fomu hii shuleni kama mwanao unampeleka shule binafsi kwa taarifa.**

5.0 Kutokana na sera ya elimu bure, tafadhali soma kwa makini maelekezo na zingatia utekelezaji wa maagizo uliyopewa kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

……

MKUU WA SHULE

TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. Jina kamili ……. Tarehe ya kuzaliwa kama inavyoonekana kwenye cheti cha kuzaliwa……(taja mwaka na mwezi)
2. Kabila ……
3. Dini na Dhehebu……..
4. Jina la Baba / Mlezi …….
5. Mahali anapoishi Baba / Mlezi (Mtaa) ……..……..Namba ya simu …….. Kazi yake ……
6. Jina la Mama/mlezi ……..…….
7. Mahali anapoishi Mama / Mlezi (Mtaa) ……..……..Namba ya simu …….…….. Kazi yake ……
8. Wazazi wanaishi pamoja au wametengana …….
9. Hali ya mwanafunzi yatima au si yatima ……..
10. Nathibitisha kwamba habari zote nilizotoa ni zakweli na sahihi.

Sahihi ya mwanafunzi ……... tarehe……

Sahihi ya Mzazi / Mlezi …… tarehe ……

HALMASHAURI YA MJI NJOMBE - SHULE YA SEKONDARI YAKOBI

SEHEMU YA MWANAFUNZI

Mimi …….…… Msichana / Mvulana ninakubali nafasi niliyopewa kuingia kidato cha …….. mwaka ……. Katika shule ya Sekondari YAKOBI na nitafika shuleni bila kuchelewa.

Nitatii na kuzingatia Sheria, Kanuni na taratibu zote za shule na za nchi.

Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kazi za elimu ya kujitegemea.

Sahihi …….. Tarehe ……..

SEHEMU YA MZAZI /MLEZI

Mimi …….…… ninakubali mtoto wangu kuingia Shule ya Sekondari Yakobi kidato cha …….. mwaka ……na ninaahidi kumpatia mahitaji yote muhimu kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na Shule (Joining instruction) na ninahakikisha kuwa nitashirikiana na uongozi wa Shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa Shule na Taifa .

Anuani yangu ya kudumu ni

……..

……..

Namba ya simu ……..

Sahihi …….. Tarehe ……..

MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by a medical officer in respect of new student

Student name in ful……..……..……...

Age …….……

Blood count (red and white)……..……

Stool examination……..

Urine analysis……..……..

Syphilis analysis……

T.B Test……..……

Ears Test ……

Eyes Test……

Chest Test ……

Spleen Test…….…..……

Abdomen Test…….…..……

Typhoid Test…….……...…

Pregnancy Test…….……

N.B (any disease discovered should be treated)

Addition information (Any physical defect or impairment, infection chronic or family disease)

……

……

……

I certify that the above is fit/un fit for admission into day/boarding school

Name……..…….signature……

Designation ……

Station ……

Date……

OFFICIAL STAMP

TANBIHI: FIKA NA FOMU UNAPORIPOTI SHULE